**Learning By Ear 2011 Biashara – "Kuanzisha Biashara"**
**Kipindi cha 9: "Kusajili"**
AUTHOR: Erick-Hector HOUNKPE
EDITORS: Yann Durand, Aude Gensbittel, Adrian Kriesch
TRANSLATOR: Anne Thomas
PROOFREADER: Charlotte Collins

## Characters

Msimulizi

Daniel Huba (Mwanamume, umri wa miaka 29)

**Scene 1:**

**KOSSI** : (Mwanamume, umri wa miaka18)

**ABBAS:** (Mwanamume, umri wa miaka 21)

**MARIAM:** (Mwanamke, umri wa miaka19)

**Mr. Masinga:** (Mwanamume, umri wa miaka 57)

**Scene 2:**

**KOSSI**: (Mwanamume, umri wa miaka18)

**ABBAS:** (Mwanamume, umri wa miaka 21)

**OFFICIAL:** (Woman, 27 years old)

**MARIAM:** (Mwanamke, umri wa miaka19)

**Scene 3:**

**KOSSI** : (Mwanamume, umri wa miaka18)

**ABBAS:** (Mwanamume, umri wa miaka 21)

**MARIAM :** (Mwanamke, umri wa miaka19)

**LINDA:** (Mwanamke, umri wa miaka 20, dadake Kossi)

**JOHN:** (Mwanamume, umri wa miaka 21, kakake Mariam)

**Learning By Ear 2011 Biashara – "Kuanzisha Biashara"**
**Kipindi cha 9: "Kusajili"**
AUTHOR: Erick-Hector HOUNKPE
EDITORS: Yann Durand, Aude Gensbittel, Adrian Kriesch
TRANSLATOR: Anne Thomas
PROOFREADER: Charlotte Collins

## INTRO

### Host:

Hamjambo na karibuni kwenye Noa Bongo Jenga Maisha Yako na kipindi kingine cha mfululizo wa vipindi vyetu kuhusu kuanzisha biashara, vinavyokuonyesha jinsi ya kujisimamia maishani. Mara iliyopita, Mjomba Masinga aliwaahidi wenzetu Abbas, Kossi na Mariam kwamba angekuwa "malaika" wao wa kibiashara; maanake angewapa msaada wa kifedha ili waanzishe biashara yao ya usanifu. Lakini alisema angefanya hayo kwa sharti moja. Ni sharti gani hilo? Utajua hayo katika kipindi hiki cha tisa kinachohusu "Usajili":

### Scene 1: At Uncle Masinga's

**Mr. Masinga, Kossi, Mariam, Abbas**

| | |
|---|---|
| **1. ATMO: Outside, birds, wind, traffic in the distance** | |
| **2. ABBAS:** | Kwa hisani yako mjomba, tupe masharti yako! Mradi tu tusiwe watumwa wako tutakubali jambo lolote jingine! **(laughing)** |
| **3. MR. MASINGA**: | Lazima mwandikishe rasmi kampuni yenu. Kampuni yenu inapaswa kuwa na misingi ya kisheria, vinginevyo siwezi kuwasaidia. |
| **4. MARIAM**: | Ni hayo tu, mjomba? |
| **5. MR. MASINGA**: | Naam, hayo tu, na msione kama kwamba ni jambo dogo. Hali ni kinyume– mtakabiliwa na usumbufu |

mwingi, ni lazima mvuke vizingiti vyote hivyo vya kufanya mambo rasmi. Kwanza mnatakiwa kujua nyaraka zinazohitajika na wakuu wa serikali kabla ya kuanzisha kampuni. Nina shughuli nyingine za kutekeleza, kwa hivyo ninaawaga. Kazi kwenu tena …

**6. SFX: Sound of chairs**

**7. KOSSI**: (**Enthusiastically**) Usiwe na wasiwasi – tutajitahidi kadiri ya uwezo wetu, na tutajaribu kuharakisha mambo …

**8. MR. MASINGA**: **(walking away)** Fanyeni bidii …

**9. SFX: Sound of steps going away (1 person)**

**10. Narrator:** **Kwa nini Bwana Masinga akashikilia kwamba wenzetu wasajili rasmi kampuni yao? Na vipi watalitekeleza hilo? Ebu tumsikilize mtaalamu wetu Daniel Huba wa Chuo Kikuu cha Inoorero mjini Nairobi:**

**11. Daniel Huba 1’05**

*Kuna njia mbali mbali za kusajiliwa biashara. Kutegemea na aina ya biashara, huenda ukaisajili biashara yako kwa kibali kimoja cha biashara au tuseme leseni. Vibali sampuli hii hutolewa na serikali za wilaya. Kwa mfano wachuuzi unaowaona na vibanda sokoni; wana vibali vya biashara moja moja. Namna nyingine ni kusajili biashara yako kwa kusema kwa mfano: ‘Haya biashara yangu imeendelea kufikia kiwango ambacho nadhani nahitaji kuwa na kampuni.’ Ukiamua kuwa na kampuni kuna gharama kadha wa*

*kadha ambazo utalipia. Hata hivyo kuna faida za kuwa na kampuni. Faida moja ni kwamba kampuni si sawa na wewe mwenye hiyo kampuni. Kwa mfano kampuni ya Safaricom Limited ya simu za mkono. Ni tofauti kabisa na Michael Joseph aliyekuwa Afisa Mkuu Mtendaji wa kampuni hiyo. Ni njia moja wapo ya kusajili kampuni na huku hujatwaa dhamana kubwa kwenye kapmuni hiyo. Aidha madeni yako yamedhibitiwa yaani kiasi unachoweza kupata hasara kwenye kampuni kimedhibitiwa.*

**12. Narrator:** Inaonekana rahisi. Tujiunge tena na marafiki zetu tusikie hatua watakazochukua.

**<u>Scene 2: At the registration office</u>**

**Official, Abbas, Mariam, Kossi**

**13. ATMO: Inside, computer keyboard, rustling of paper, people talking in the background**

**14. OFFICIAL**: Basi, kama ambavyo nimekwambia, masharti si magumu. Kwanza mnatakikana mjumuishe kila kitu kinachohitajika ili mfunguliwe jalada. Kila mwanzilishi wa kampuni anatakikana kuleta nakala tano za cheti chake cha kuzaliwa, nakala tano za hati ya taarifa za idara ya upelelezi wa jinai, na cheti cha usajili ambacho unakipata kwetu kwa kulipa dola tano. Kisha utajaza cheti hicho na kutia sahihi. Tunahitaji pia taarifa zako za ulipaji kodi za muda wa miaka mitatu iliyopita, kibali chako cha ukazi, risiti inayoonyesha

kwamba umelipa kodi katika mwaka wako wa kwanza wa biashara, - unaweza kulipa katika afisi ya kodi, shubaka la tatu … Zaidi ya hayo, ni lazima upate risiti ya arbuni ya kuanzisha biashara. Ada yake ni baina ya dola 500 na 5,000 kulingana na kampuni unayotaka kuanzisha.

15. **SFX**: Sound of paper changing hands

16. **OFFICIAL**: Nadhani kabrasha hili litakufaa. Taarifa zetu za benki zimeandikwa humo. Aaa nimesahau – inakubidi kupeana nakala tano za nyaraka zako za binafsi – nyaraka asili pamoja na nakala nne. Nenda uzipeane kwenye shubaka nambari 12 …

17. **MARIAM**: (**Panicking**) Lakini mama! Yote hayo kabla hatujaanzisha kampuni! Unataka kutuangamiza?

18. **ABBAS**: Inaonekana kana kwamba hakuna mtu anayewataka vijana wajihusishe na biashara humu nchini! Kama huu si wazimu ni nini … Kulipa kodi hata kabla ya kuanzisha kampuni?! Lipa hiki lipa kile!

19. **OFFICIAL**: (**loudly**) Mwingine tafadhali! (**To our friends**) Vijana, kwani hamuoni, watu wanaosubiri ni wengi, na mwenyewe nina kazi za kufanya …

20. **SFX: Sound of chairs, steps going away (3 people)**

**21. ABBAS**: (**Really annoyed**) Balaa! Mambo makubwa! Sasa ndio nini! (**Complaining**) Hivyo ndivyo watu hukaribishwa! Upumbavu ulioje!

**22. SFX: Door opens slams**

**23. ATMO: Traffic, beeping**

**24. MARIAM**: HAYA, tupunguzeni hasira.

**25. ABBAS**: Una maana gani, tupunguze hasira? Siwezi! Haya yanavunja mtu moyo! Yanakatisha tamaa kabisa -…

**26. MARIAM**: **(interrupting)** Ebu tumakinike la sivyo hatutafaulu kutimiza mradi wetu. Ni jambo gumu kwa kweli. (S**ilence**)

**27. KOSSI**: Lakini umemsikia huoy mpumbavu, umehisi jinsi alivyo na kiburi?

**28. MARIAM**: Naam, lakini ninamhurumia – yeye kazi yake kuwa afisini na kufanya mambo kutegemea kanuni zilizowekwa. Halaumiki kwa vyovyote vile kwani ndivyo mfumo unavyotaka.

**29. ABBAS**: (**Calm again**) HAYA jamaa, twendeni zetu – tuna kazi nyingi za kufanya.

**30. KOSSI**: Naam, tunahitajika kwenda mahali pengi – mahakamani kwa taarifa za jinai, kwenye afisi za manispaa kupata vyeti vya kuzaliwa, na pia kupata vibali vyetu vya ukazi. Na nadhani tutatumia muda

mwingi hasa tukizingatia kasi ya kutekeleza mambo hapa, na pia na hao matapeli ambao watakuwa tayari kutulaghai …

**31. MARIAM**: Bora tujiandae vizuri kwa hili jambo. Mmoja wetu atakwenda kuchukua taarifa za jinai, mwengine vyeti vya kuzaliwa. Jamani hatuna muda wa kupoteza! Kama walivyosema wahenga : " Penye nia pana njia!" Na endapo kutakuwa na tatizo lolote tutashauriana tena na Mjomba Masinga …

**32. Narrator:** **Baadhi ya matatizo huoenekana magumu kuyakabili unapoanza jambo. Fomu, nyaraka rasmi, kodi, arbuni– vitu vyote hivyo mara nyingine huwakatisha tama watu. Hata hivyo bora kuvumilia, kama anavyosema mtaalamu wetu Daniel.**

**33. Daniel Huba 1'05**

*Ninafahamu kwamba wafanyabiashara wanakabiliwa na changamoto nyingi. Mara nyingine tunaogopa kulipa kodi, tunaogopa kutenda mabo kirasmi kwa sababu tunakisia kwamba ni ghali sana. Biashara haziwezi kutekelezwa daima bila kufanywa rasmi. Kuna wakati ambapo biashara yako inaimarika. Na kama biashara yako inaimarika vyema uwe tayari kuisajili rasmi. Na unapoisajili uwe tayari kulipa kodi, ili upewe nambari ya ulipaji kodi. Hizi ni hatua muhimu sana. Kwasababu ukitaka kupata kandarasi zaidi, biashara nzuri zaidi ni lazima ugharamike. Si rahisi. Lakini pia inakubidi uwe mwepesi wa kutafuta ushauri, naam, tafuta ushauri kabla ya kuisajili biashara yako!*

**34. Narrator:** Marafiki zetu hawakukata tamaa na bidii yao imewaletea ufanisi. Siku chache baadaye walikuwa wameshavuka vizingiti vyote kwa msaada wa Mjomba Masinga. Aidha wamefanikiwa kupata mahali pa kufungua afisi ya kampuni yao. Tunaungana na Abbas, Mariam na Kossi majuma matatu baadaye…

## Scene 3: At the Young Design offices in the town center

**Mariam, Abbas, Kossi, John, Linda**

**35. ATMO: Interior atmosphere, fan, traffic outside**

**36. SFX: Sound of furniture (desk) being moved around**

**37. ABBAS**: **(Out of breath)** Hapana, sidhani hivyo. Utasimamia mawasiliana, wala si uhusiano wa umma. Sijui kwa nini dawati lako liwe karibu na mlango.

**38. MARIAM**: Kwa ni lazima nionekane, na lazima nimuone kila aingiaye na atokaye.

**39. KOSSI**: Madawati yote matatu yanatakikana kuwa upande wa nyuma kama tulivyokubaliana awali.

**40. MARIAM:** Sijakubali, lakini wengi wape.

**41. ABBAS**: (**A little smile**) Hutaki dawati lako likaribiane na langu?

42. **MARIAM**: Hapana, sivyo, hutanisababisha nisiweze kufanya kazi vizuri.

43. **KOSSI**: Ah ha! Sasa nimetambua! (**burst of laughter**) Tulieni! Mwaonaje tukiangika leseni mkabala na mlango wa kuingilia ili kila aingiaye aione kwa urahisi?

44. **MARIAM**: Sawa hivyo, kila mtu anapaswa kuona kwamba sisi si malimbukeni tu, tuna kibali. Iweke hapo!

45. **SFX: Sound of nail pounded in the wall**

46. **ABBAS**: Naam, vizuri hivyo. Ndiyo, hapo, sawasawa.

47. **SFX: Door opening**

48. **JOHN and LINDA**: (**Enthusiastically**) Wow!!!

49. **MARIAM**: Oh, mambo vipi, John na Linda - nawaona… mmefika wakati ufaao ili tuwatembeze afisini kwetu!

50. **JOHN**: Inapendeza si haba!

51. **SFX: Sound of steps**

52. **LINDA**: Aha, jamaa wa fedha amejificha pembeni. Mkakati mzuri huo. Nadhani Afisa Mkuu Mtendaji atakaa katikati, akiangaza yote yatakayofanyika kote afisini. Lakini hapana chumba cha mapokezi …

53. **ABBAS**: Mkakati pia huo, Hakuna kusubiri hapa pindi mtu anapoingia!

54. **KOSSI and MARIAM**: (**In chorus, like a slogan**) Hakuna kusubiri hapa! Pindi unawasili, uanhudumiwa mara moja! (**Everybody bursts out laughing, clapping**)

55. **KOSSI**: Kule nyumba, nafasi hiyo iliyozingirwa, ni chumba cha mikutano. Nifwateni.

56. **SFX: Sound of steps, of doors opening and closing**

57. **LINDA**: Ah ha! Kwa hivyo hapa ndipo mahali pa kutafakari …

58. **JOHN**: Afisi nzuri kwa kweli!

59. **ABBAS**: (**A little bit emotional**) Lakini sasa ndio kazi ngumu inaanza. Msisahau – kama alivyopenda kusema mwalimu wangu wa falsafa, "Tunapotimiza lengo, tunaanza tena, maana kuna lengo jipya kwenye upeo…"

60. **MARIAM**: (**Finishing**) … tutakuwa wajinga wa mwisho tukikinai kwa hili lengo bada ya kuzingatia lengo". Mwisho wa nukuu.

61. **KOSSI**: Kweli. Hata kama mapambano mapya yatakuwa magumu, ninajua yatakuwa mazuri na tutashinda mwishowe.

62. **MARIAM:** Inshaallah! Tuishangilieni Young Design! (**They start cheering and clapping)**

63. **ABBAS**: (**Happy**) *Young Design* imezaliwa! (**The applause and laughter begins again.)**

## OUTRO:

### Host:

Na huo ndio mwisho wa kipindi cha tisa cha mfululizo wetu wa vipindi vya Noa Bongo Jenga Maisha Yako kuhusu kuanzisha biashara, vinavyomshirikisha Daniel Huba wa Chuo Kikuu cha Inoorero nchini Kenya. Kampuni imeanza vizuri. Lakini je biashara itawaendea vyema Mariam, Abbas na Kossi? Sikiza kipindi kijacho upate taarifa zaidi. Una maoni gani kuhusu mtu kusajili biashara yake? Unadhani ni sawa marafiki zetu walivyofanya? Tueleze uzoefu wako, kwa barua-pepe kupitia anwani kiswahili@dw.de

Ukitaka kukisikiliza tena kipindi hiki, au vipindi vinginevyo vya Noa Bongo Jenga Maisha Yako, tembelea wavuti yetu, www.dw.de/Kiswahili

Kwaheri kwa sasa!

**END**